TANGAZO LA SERIKALI NA. 705 tarehe 22/9/2023

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,
(SURA YA 414)

# NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha. 19)*

NOTISI YA UCHUNGUZI KUHUSU YA MAOMBI YA BEI ZA MAJI YA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA NZEGA YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uchunguzi ya Maombi ya Bei za Maji ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Nzega ya Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Notisi hii, Isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka; na

"uchunguzi" maana yake ni mchakato mzima wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu marekebisho ya bei yanayopendekezwa kama inavyooneshwa kwenye Majedwali ya Kwanza, Pili, Tatu, Nne na Tano ya Notisi hii.

Madhumuni ya uchunguzi

3. Madhumuni ya uchunguzi ni kuiwezesha Mamlaka kukusanya maoni ya wadau kuhusu bei zinazopendekezwa.

Mapendekezo ya bei

4. Bei zinazopendekezwa na Nzega WSSA zimeoneshwa kwenye Majedwali ya Kwanza, Pili, Tatu,

Nne na Tano ya Notisi hii.

Jinsi ya kushiriki katika uchunguzi

5. Mtu anayetaka kushiriki kwenye uchunguzi anaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anwani iliyotajwa katika aya ya 8 ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Pingamizi

6. Mtu mwenye nia ya kuwasilisha pingamizi dhidi ya kuidhinishwa kwa maombi ya bei atawasilisha pingamizi lake kwa maandishi ndani ya siku tano za kazi baada ya siku ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Nakala za Maombi

7.-(1) Nakala za maombi ya bei ya Nzega WSSA zinapatikana kwenye ofisi za Mamlaka saa za kazi kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni kwa ajili ya taarifa kwa umma.

(2) Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu kupitia anwani iliyotajwa kwenye aya ya 8.

Anwani ya Mamlaka

8. Anwani ya Mamlaka itakuwa-
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,
Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104, Tambukareli,
S.L.P. 2857,
Dodoma.
Barua Pepe: info@ewura.go.tz

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 1,500 | 2,610 | 2,891 | 2,974 |
| Taasisi | 1,670 | 2,906 | 3,219 | 3,311 |

*Tangazo La Serikali Na. 705 (Linaendelea)*

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Biashara | 1,800 | 3,132 | 3,470 | 3,568 |
| Viwanda | 1,800 | 3,132 | 3,470 | 3,568 |
| Magati | 1,250 | 2,175 | 2,410 | 2,478 |
| Wastani | 1,480 | 2,643 | 2,928 | 3,011 |

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 15,000 | 20,000 | 25,000 | 30,000 |
| Taasisi | 15,000 | 25,000 | 30,000 | 35,000 |
| Biashara | 15,000 | 25,000 | 30,000 | 35,000 |
| Viwanda | 15,000 | 25,000 | 30,000 | 35,000 |

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Asilimia 20 ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Uondoaji wa Majitaka (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | - | 15,000 | 18,000 | 18,000 |
| Taasisi | - | 15,000 | 18,000 | 18,000 |
| Biashara | - | 20,000 | 25,000 | 25,000 |
| Viwanda | - | 30,000 | 30,000 | 30,000 |

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kumwaga Majitaka kwenye Mabwawa ya Nzega WSSA kwa Magari Binafsi (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Magari Yote | - | 2,000 | 2,000 | 2,000 |

Dodoma, JAMES A. MWAINYEKULE

.............................., 2023 *Mkurugenzi Mkuu*